

Kuunda Mpango wa Elimu Iliyobinafsishwa kwa ajili ya Mtoto Wangu



Baada ya mtoto wako kutambuliwa kustahiki kwa elimu maalum, shule itaunda mpango nawe ili kuhakikisha kuwa mtoto wako ana usaidizi wa mafunzo na hisani anazohitaji ili kupokea elimu inayofaa. Mpango huu unaitwa Mpango wa Elimu Iliyobinafsishwa (Education Program, IEP).

Je, IEP ya mtoto wangu inaundwa vipi?

- Shule ya mtoto wako itakualika ili ushiriki katika mkutano wa IEP kuunda mpango kila mwaka. Wengine kwenye timu wanaweza kujumuisha walimu wa mtoto wako, mwakilishi kutoka kwenye wilaya ya shule, mwanasaikolojia wa shule na wataalamu wengine.
- **Mtoto wako anahimizwa kuhudhuria na hata kuongoza mikutano ya IEP.** Hatua hii ni muhimu haswa ikiwa mtoto wako amekomaa na yuko kwenye shule ya upili.
- **Unaweza kumwalika yeyote aliye na maarifa au umahiri kuhusu mtoto wako kwenye mkutano wa IEP wa mtoto wako, ikiwemo mhudumu wako wa jamii.**
- **Lazima shule ziwe na mkalimani wa lugha yako ya asili kwa ajili ya mkutano huu.**

Je, ni nini kinachotendeka baada ya mkutano wa IEP?

Pindi tu timu inapounda IEP, lazima shule ya mtoto wako ifuate IEP kwa kumpa mtoto wako huduma na usaidizi ulioelezwa ndani yake. Timu ya IEP itakutana angalau mara moja kwa mwaka ili kupitia na kusasisha IEP. Ikiwa unataka kukutana baina ya mikutano ya kila mwaka ya kawaida, unaweza kuwasilisha ombi la maandishi kwenye shule kwa mkutano wa IEP wakati wowote. Lazima shule iratibu mkutano ndani ya siku 45 za shule baada ya ombi lako.



Ikiwa mtoto wako hastahiki kwa IEP, anaweza kupokea **Mpango wa 504**. Pata maelezo zaidi **kuhusu Mipango ya 504** katika mwongozo wetu kwenye *Je, Ikiwa Mtoto Wangu Hastahiki Elimu Maalum?*